



## Sare ya Shule

*Cha shule:*
Shati la Bluu lenye Kola
Suruali / sketi za kaki au nyeusi
*Kwa Elimu ya Mazoezi ya Viungo:*
Shatitao la FLC
Suruali au kaptura za jasho

## Kitambulisho




Ni lazima uwe na Kitambulisho chako kila mara. Usiharibu Kitambulisho chako. Sahau Kitambulisho chako = lipa $1
Poteza

Kitambulisho

## Vifaa vya Shuleni

Tano (5) 1-Madaftari ya Masomo
Penseli / Kalamu za wino
Folda




## Saa za Shule

*Shule hufunguliwa kwa kiamshakinywa:*
**7:15 – 7:45 asubuhi**
*Masomo Yanaanza:*
**7:55asubuhi**
*Masomo kumalizika:***2:59 jioni**
(Jumatatu, Jumanne, Alhamisi, Ijumaa)
*Masomo kumalizika:*
**1:59 jioni** (Jumatano)

**Kiamshakinywa cha bila malipo**
**Chamcha cha bila malipo**
**SEPTA Transpassbila malipo**
(basi / toroli / reli ya chini)
**Iwapo unaishi maili 1.5mbali na shule**
Pata Transpass wakati wa Jumatano/Alhamisi/Ijumaa ya Ushauri
**Tarehe za Kadi ya Ripoti**:
Novemba 20, 2017
Februari 14, 2018
Mei 2-4, 2018
Juni 12, 2018
**Tafsiri / Ukalimani**
215-400-4180, ext. #4

# Newcomer Learning Academy (NLA)



## Franklin Learning Center (FLC)

616 N. 15th Street
Philadelphia, PA 19130
215-400-7570

Ofisi ya Mtaala na Mipango ya Lugha Mbalimbali Wilaya ya Shuleya Philadelphia /
215-400-4240

# Karibu katika NLA kwenye FLC







Newcomer Learning Academy (NLA) ni ya wanafunzi walio na:

- Mmiaka 14 – 20,
- Waliowasili hivi karibuni Marekani, na
- Wanazungumza lugha ya kwanza mbali na Kiingereza.

Wanafunzi wanajisajili kupitia Kituo cha Kutathmini Lugha Mbalimbali (Multilingual Assessment Center,MAC): 215-400-4240 (Chaguo la 1). Iwapo mwanafunzi ana hati ya shule, itaweza kupelekwa katika Ofisi ya FLC Roster au MAC.

Mahitaji ya kufuzu ya Shule ya Wilaya ya Philadelphia ni alama 23.5: Kiingereza (4), Historia/Sayansi ya Jamii (4), Hisabati (3-4), Sayansi (3-4), masomo ya sanaa (2), vichaguliwa (4), elimu ya mazoezi ya viungo (1) afya (.5), na lugha ya ulimwengu (2).

Kuhudhuria ni muhimu sana. Iwapo hujaja shuleni, unahitajika kuwa na barua iliyotiwa sahihi na mzazi/mlezi wako. Iwapo hujaja kwa zaidi ya siku 3+, unahitaji kuwa na barua kutoka kwa daktari. Kutokuja “kunakoruhusiwa” ni kwa ugonjwa, kifo katika familia, mandari ya shule, au likizo ya dini katika familia. Iwapo una maswali, tafadhali zungumza na mwalimu wako Mshauri.

Iwapo “utaagizwa kuondoka mapema,” (ondoka mapema) unahitajika kuwa na barua kutoka kwa mzazi/mlezi wako. Iwapo hujafikisha miaka 18, lazima mzazi/mlezi wako aje akuchukue. Anapaswa kuwa na Kitambulisho chenye picha.

Iwapo unaugua, tafadhali mwambie mwalimu wako. Ikiwa unakunywa dawa, lazima umpe dawa mwuguzi aliye katika Chumba 111.

NLA ina walimu 8, mshauri wa shule na Washauri Wasaidizi wa Lugha Mbili (Bilingual Counseling Assistants, BCA). Mshauri wa shule anaweza kusaidia kwa mipango ya chuoni na ajira usaidizi wa kijamii/hisia. BCA itasaidia kwa tafsiri, huduma za kijamii na misaada ya jamii.

Matokeo ya tabia hasi ni pamoja na “kizuizi.” Kizuizi ni nyongeza au saa ya ziada baada ya shule kwa wanafunzia mbao:

- Wamechelewa kuja shuleni au darasani,
- “mkato” wa darasa (usiende darasani), na/au
- Kushiri kitabiahasi (mbaya) katika darasa, barabara za kumbiza shuleni, bwalo, katika mandari ya shule, kuenda na kuja shuleni, nk.

## Sheria za NLA/FLC

**Ndiyo kupata** rafiki wapya, kufikiria, kuuliza maswali na kujifunza! **Ndiyo** kujiunga na vilabu, vikundi vya muziki na kucheza michezo!



**Simu za Mkono Haziruhusiwi darasani**



**Kofia au Fulana zenye Kofia haziruhusiwi shuleni**

**Kuvuta sigara, kunywa pombe au mihadarati haviruhusiwi shuleni**



**Zana Haziruhusiwi**
**Silaha Haziruhusiwi**

